**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 30 Mei, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

113. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ:

Majeshi yetu kama vile Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kikosi cha Valantia (KVZ) na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ni majeshi yaliyoanzishwa kupitia sheria zilizotungwa hapa Zanzibar. Moja kati ya jambo ambalo ni kikwazo kikubwa katika majeshi yetu haya ni mavazi kwa wanajeshi wa kike. Kumekuwa na malalamiko makubwa kwa walinzi wetu wa kike kukosa haki 13 ikiwa ni pamoja

na haki yao ya kuvaa hijabu pamoja na kufunika nywele zao wanapokuwa katika majukumu yao ya kila siku.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuwaruhusu wanawake wanaohudumu katika vikosi hivi kuvaa vilemba maalum vinavofunika vichwa vyao ili kuendana na mila na desturi za Mzanzibari.

(b) Je, tathmini inaonyesha ni wanawake wangapi walioajiriwa katika majeshi yetu haya na katika vyeo gani.

(c) Kwa kuzingatia kuwa majeshi haya yameanzishwa kupitia sheria za Zanzibar, Je, Serikali ina sera au mikakati yoyote inayolenga kutatua changamoto za mavazi kwa wanajeshi wa kike.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

110. MHESHIMIWA. DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tarehe 21 Novemba 2023, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia taasisi zake sita (6), iliingia makubaliano na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kuipa fursa NBC kukusanya malipo ya Serikali mbali mbali kupitia mfumo na mtandao wa kidigitali wa benki hiyo.

(a) Je, makubaliano hayo na NBC yamelenga katika maeneo gani ya ukusanyaji wa mapato.

(b) Je, ni mchakato gani uliotumika mpaka kuipata Benki ya NBC na kumpa kazi ya ukusunyaji wa mapato ya Serikali.

(c) Je, ni muda gani utekelezaji wa makubaliano haya utaanza kufanyika, na ni upi mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kuna uwazi katika ukusanyaji huo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

213. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa michezo ni ajira, je ni mikakati gani ambayo Wizara yako kwa kushirikiana na ZFF inaichukua katika kuona kwamba tunauza vipaji kwa wingi nchi za nje na kupunguza ununuaji wa wachezaji kutoka nje kuja nchini kwetu.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

195. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni utaratibu upi unaotumika katika maandalizi na maamuzi ya kuitangaza misitu ya hifadhi iliyopo Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

66. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na Wizara hii kupongezwa juu ya huduma bora wanazozitoa kwa wagonjwa wanaofika katika hospitali ya Kivunge, bado yako malalamiko yanayohusiana na manyanyaso wanayoyapata wananchi hao hasa wanaofika kupata huduma katika nyakati za usiku.

Ni lini wanaohusika na manyanyaso hayo watachukuliwa hatua za kinidhamu.

144. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi): Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika kuboresha huduma bora za afya kwa jamii, Wizara ya Afya imeanzisha mfumo unaorahisisha taarifa za mgonjwa kuweza kusomeka na kufahamika katika kila eneo la hospitali husika, kutoka mapokezi hadi kwenye eneo la dawa na kwengineko ili kuendana na wakati.

(a) Je, ni kwa kiasi gani mfumo huu umeweza kurahisisha upatikanaji wa huduma kulingana na dhamira iliyokusudiwa.

(b) Je, ni kwa kiasi gani watendaji wamepatiwa mafunzo ili kuweza kuendana na lengo lililokusudiwa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

83. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na azma ya muda mrefu sasa ya kuzijenga barabara zilizojengwa kwa lami baridi kama vile

barabara ya Mtambile, Mwambe – Kangani, Mizingani – Wambaa, Kenye – Chambani na nyenginezo, lakini mpaka sasa zimekuwa na hali mbaya ya kupitika.

(a) Je, kuna sababu zipi zilizopelekea barabara hizi kutokujengwa hadi leo.

(b) Je, wananchi wategemee barabara hizo zitajengwa lini.

135. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na kadhia katika bandari ya Dar es Salaam kwa muda mrefu sasa kwa abiria wanaosafiria meli za usiku kuja Zanzibar, hupekuliwa mizigo yao kwa kutumia mbwa, kitendo ambacho ni kinyume na imani za wananachi wengi. Jambo hili limekuwa likilalamikiwa na abiria wengi kwamba linawadhalilisha na kuwaweka katika wakati mgumu kwa mujibu wa imani zao.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili na ni hatua gani imechukua kulitatua ili kuepusha taharuki kwa wasafiri.

(b) Je, ni upi utarataibu wa ukaguzi wa mizigo inayoingia Zanzibar kupitia bandari ya Dar es salaam.

(c) Je, Serikali ina taarifa kutoka Mamlaka za Bandari ya Tanzania (TPA) kuhusu lini bandari hiyo itawekwa mashine za ukaguzi ili kuwapunguzia wasafiri usumbufu wa kadhia hii.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

148. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania (SMT) imekuwa ikitekeleza mradi mkubwa kutoka Benki ya Dunia wa HEE (High Education for Economic Transformation) kwa taasisi za elimu ya juu kwenye maeneo tofauti. Pamoja na mradi huu kusimamiwa na SMT, kuna taasisi chache tu za elimu zilizobahatika kunufaika na mradi huu.

(a) Je, ni taasisi ngapi zilizopata ufadhili wa mradi huu baina ya Tanzania Bara na Zanzibar na kiasi gani cha fedha watakazopata.

(b) Je, ni sababu zipi zilizopelekea taasisi chache kupata ufadhili huu kwa Zanzibar ukilinganisha na Tanzania Bara.

190. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Je, Shule Jumuishi za Watu Wenye Mahitaji Maalum zina mchango gani katika kuibua vipaji vyao na kuviendeleza.

(b) Ni kwa kiasi gani mpango mkakati wa kupatikana vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika skuli zetu unatekelezwa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2024/2025.

**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2024/2025.



**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**30 Mei, 2024.** **KATIBU WA BARAZA**